

TANROADS YATOA ELIMU KUHUSU VIFAA VYA KUHE SABU MAGARI BARABARANI (INDUCTIVE LOOP VEHICLE COUNTERS)

WAKALA ya Barabara Tanzania (TANROADS) imetoa elimu maalum kwa wadau wa usafirishaji na umma kwa ujumla, kuhusu vifaa maalumu vya kuhesabu magari vinavyojulikana kitaalamu kama **'INDUCTIVE LOOP VEHICLE COUNTERS'** ambavyo vimevifungwa katika barabara kuu za mikoa yote nchini, lengo lake kubwa ikiwa ni kuhakikisha takwimu sahihi za magari yanayopita katika barabara hizo.

Akizungumza na Wanahabari jijini Dar es Salaam, katika ziara ya kukagua kifaa kimojawapo kilichofungwa katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Meneja wa Mifumo ya Usimamizi wa Rasilimali za Barabara TANROADS, Mhandisi Mussa George alisema, vifaa hivyo ambavyo vimefungwa miezi miwili iliyopita vinatumika kupima aina ya gari na idadi na sio mwendokasi wa gari husika.

Aidha, alisisitiza TANROADS imefunga vifaa vya kuhesabia magari ili kupata takwimu sahihi na kupunguza gharama, kwani hapo awali zoezi hili lilihusisha watu kwa ajili ya kuhesabu na hivyo kupelekea kutokupatikana kwa takwimu sahihi.

"Teknolojia inazidi kukuwa, TANROADS imekuwa ikihesabu idadi ya magari kupitia watu sasa kifaa hiki kinatusaidia kupata takwimu halisi, kifaa hiki kitakuwa hapa kwa saa 24" alisema.

Aliongeza "Lengo la kuhesabu magari ni kupata takwimu za magari zitakazotusaidia kwa ajili ya usanifu na matengenezo ya barabara, siku zote unapofanya usanifu wa barabara lazima ujue idadi na aina ya magari yanayopita katika barabara hiyo," alisema.

Alisema, TANROADS tayari imenunua vifaa 150 na vimefungwa nchi nzima katika barabara za lami na wameanza kwa majaribio kuziweka katika barabara kuu.

"Dar es Salaam ndio jiji lenye magari mengi zaidi hivyo, tumefunga vifaa 16, kuna mikoa mingine imepata vifaa 10, vifaa hivyo vitadumu ndani ya maeneo yaliyowekwa, vina uwezo mkubwa wa kuhisi na kuhesabu gari kulingana na muelekeo wake," alieleza.

Mhandisi George alisema, ufungwaji wa vifaa hivi vya kuhesabu magari (INDUCTIVE LOOP VEHICLE COUNTERS) ni njia mojawapo ya TANROADS kufanya maboresho katika miundombinu ya barabara, kuendana na mahitaji ya kiteknolojia.

Aidha, alibainisha kuwa, ununuzi na ufungaji wa vifaa hivyo umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 3 na hivyo alitoa rai kwa wataanzania kuisaidia TANROADS katika utunzaji wa miundombinu hiyo, na kutoa taarifa yoyote ya uhujumu kwa Polisi au Mameneja wa TANROADS ili kusaidia kulinda miundombinu ya barabara kwa maslahi mapana ya taifa.